

Jina..... Nambari yako...../.....  
Shule..... Tarehe .....

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3

(INSHA)

JULAI / AGOSTI / 2012

MUDA: SAA 2 1/2

**MTIHANI WA TATHMINI WA PAMOJA YA SHULE ZA WILAYA YA BURETI- 2012**  
**Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari (KCSE)**

**MAAGIZO**

1. Jibu maswali manne.
2. Swalii la kwanza ni la lazima.
3. Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu ya B,C,D na E.
4. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

**Kwa matumizi ya mtihini pekee.**

swali	upeo	alamu	mtahini
1	20		
2	20		
3	20		
4	20		
5	20		
6	20		
7	20		
<b>Jumla</b>			

## SEHEMU YA A

### 1. Swali la lazima ushairi.

Soma shairi hili kisha ujili maswali yanayofuata :

#### **Kila Mchimba Kisima**

*Musa Mzenga*

1 Tenda utendapo tendo, tendo tendo kwa hekima,

Liandamane rnwenendo, sawa na yako kalima,

Kalima yenye upendo, kufurahisha mtima,

Kila mchimba kisima, budi hungia mwenyewe.

2 Utendapo la faraja, tendo ni yako salama,

Ya kukupa kila tija, na ushindi wa daima,

Upate njema daraja, duniani na kiyama,

Kila mchimba kisima, budi hungia mwenyewe.

3 Utendapo la miuja, tendo ni yako nakama

Ya kukutia harija, hasara kukuandama,

Usione afuwaja, mwanzo na yako hatima,

Kila mchimba kisima, budi hungia mwenyewe.

4 Nakwambia uelewe, pulika ninayosema,

Si ari ya mwenginewe, kumuonya kwa lazima,

Mtu hufunza mwanawe, kwanza ajue heshima,

Kila mchimba kisima, budi hungia mwenyewe.

5 Nisipokwambia wewe, kukufunza kila jema,

Kusudi nikuongowe, uepukwe na tuhuma,

Matusi ndimi nipawe, ila na kila lawama,

Kila mchimba kisima, budi hungia mwenyewe.

6. Hii si heri ujuwe, matusi kunigandama,

Hadhi usiniuzuwe, hamithishwa na nyama,

Fikiri rnoyo utuwe, nikupapo taaluma

Kila mchimba kisima, budi hungia mwenyewe.

7 Shika tena utambuwe, wasia huu ni mwema,

Matendo usipunguwe, mazuri kutenda hima,

Yatende ubarikiwe, upawe na taadhima,

Kila mchimba kisima, budi hungia mwenyewe.

8 Yakupasa uchunguwe, kila jambo kulipima,

Upime ufafanuwe, mambo yote kwa alama,

La kuwaka ulijuwe, pia lipi la kuzima,

Kila mchimba kisima, budi hungia mwenyewe.

- (a) Eleza maudhui ya shairi hili. (alama 4)
- (b) Ujumbe unaowasilishwa katika shairi hili una hadhira lengwa tatu. Zitaje na utoe mifano. (alama 6)
- (c) Eleza umuhimu wa kipokeo kinachotumiwa katika shairi hili. (alama 4)
- (d) Andika ubeti wa tano kwa lugha ya nathari. (alama 4)
- (e) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyonumiwa katika shairi:  
(i) afuwaja (alama 2)  
(ii) taaluma (alama 1)
- (f) Nakili utao wa mloto wa ubeti wa tatu (alama 1)

**SEHEMU YA B**

**RIWAYA**

S.A. MOHAMMED ; Utengano.

2. ``...Voti zenzinastahili mtu mwenye sifa mlizotaja. Mnahitaji mtumishi kama mimi.
- (a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama.4)
- (b) Fafanua sifa nne alizosema anazo mzungumzaji. (alama.4)
- (c) Sifa za mzungumzaji hazistahili kiongozi mwema. Thibitisha (alama.4)
- (d) Uhuru walionao jamii hii ni wa bendera tu. Huku ukitoa mifano,jadili ukweli wa kauli hii. (alama.8)

**au**

3. ``Mwiba wa kujichoma hauna kilio.'' Huku ukizingatia wahusika wowote watano katika riwaya ya utengano, thibitisha ukweli wa methali hii. (alama.20)

**SEHEMU YA C****TAMTHILIA****KITHAKA WA MBERIA : Kifo kisimani**

4. ``Mmojawapo wa mikono mirefu ya Butangi umekwaruzwa kidogo.''

- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama.4)  
(b) Tambua mbinu mbili za lugha zilizotumika katika dondoo hili. (alama.4)  
(c) Fafanua sababu sita zilizopelekea mapinduzi katika nchi ya Butangi (alama.12)

**au**

5. Fafanua kwa kutolea mifano matumizi ya mbinu , ya jazanda katika tamthilia ya kifo Kisima

**SEHEMU YA D****HADITHI FUPI****Mayai Waziri wa Maradhi**

6. `Hii ni dunia ya dua la kuku halimpati mwewe ! ``Alijiambia.

- (a) Ele za muktadha wa dondoo hili ( Al 4)  
(b) Ukrejelea hadithi husika, onyesha vile dunia hii ni ya , 'Dua la kuku. (Al 16)

## SEHEMU YA E

### FASIHI SIMULIZI

7. (i) (a) Eleza kwa tina maana ya neno wi mbo katika fasihi simulizi (Al 2)
- (b) Taja mambo matatu yanayopambanua muundo wa nyimbo. (Al 2)
- (c) Eleza ain a hizi za nyimbo katika fasihi simulizi. (Al 5)
- (i) Vave
- (ii) Tahalili
- (iii) Kimai
- (iv) Nyimbo za watoto
- (v) Bembea
- (d) Ingawa nyimbo ni nzuri, zina ubaya wake .  
Fafanua huku ukitoa mifano. (Al 5)
- (ii) Eleza changamoto tano zinazokabili ukusanyaji na uhi fadhi wa fasihi simulizi. (Al 5)

For More Free KCSE past papers visit [www.freekcsepastpapers.com](http://www.freekcsepastpapers.com)